

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2017/2018, MWEZI JANUARI 2018.**

**1.0 UTANGULIZI**

Katika msimu wa Kilimo 2017/18 Halmashauri ya Wilaya imeendelea kusimamia vitalu vya miche ya korosho, usambazaji wa mbegu na ugawaji wa miche. Katika msimu wa 2017/18 Halmashauri kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania imegawa /imesambaza Jumla ya miche 135,310 kwenye vijiji 30 na vijiji 17 vinavyoendeleza zao la Korosho ambavyo ni Mazae, Berege, Chitemo, Chinyika, Lukole, Kingiti, Iyenge, Nghambi, Kibakwe, Ikuyu, Pwaga, Ilolo, Pwaga, Kisokwe, Kazania, Kimagai na Idilo hadi kufikia mwezi Januari.

**2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MSIMU WA 2017/2018, CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA**

NA .	SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA	UTEKELEZAJI MSIMU WA 2017/2018	CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA
1.	Kutoa huduma za ugani katika zao la korosho	Jumla ya Maafisa Kilimo 24 wa ngazi ya vijiji na kata wamepatiwa elimu ya kilimo bora cha zao la korosho na udhibiti wa magonjwa kwa vitendo katika shamba la magereza Mpwapwa	-Upungufu wa fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wataalam wa Kilimo na Wakulima.
		Jumla ya mashamba darasa 62 yameanzishwa katika shule ya za Sekondari na Msingi <b>(Kiambatanisho A)</b>	-Uelewa mdogo juu ya upandaji na uchimbaji wa mashimo.  -Maandalizi duni kwa baadhi ya Shule za msingi na Sekondari.
2.	Usimamizi wa vikundi vya uzalishaji wa miche ya korosho	Jumla ya miche 222,450 imesambazwa na Vikundi 7 vya Gereza Mpwapwa, Wilunze Korosho, Kenet Group, Anacardium Group, Helena Malima, Good Hope na WARC Kibakwe na bado usambazaji unaendelea	-Bodi Kuchelewa kulipa vikundi 30%  -Upungufu wa vitendea kazi mf. Keni za kumwagilia.
		Usambazaji wa miche ya korosho 135,310 umefanyika katika vijiji 47 ambapo Jumla ya wakulima 2,349 wamepanda mikorosho na Jumla ya ekari 5,445 Zimepandwa, Kazi ya usambazaji miche inaendelea <b>(Kiambatanisho B)</b>	-Bajeti ndogo kwa ajili ya usambazaji wa korosho.  -Baadhi ya maeneo kushindwa kupelekewa mikorosho kutokana na kuharibika kwa miundombinu

3.	Usimamizi na ukaguzi wa miradi ya Upandaji wa miti ya mikorosho inayofadhiliwa na TASAF awamu ya III	Usimamizi na Ufuatiliaji wa miradi ya upandaji wa miti ya mikorosho umefanyika katika vijiji 14 vya Gulwe, Kingiti, Iyenge, Makose, Chogola, Kimagai, Inzomvu, Makutupa, Bumila, Mazae, Mwanakianga, Idilo, Mwenzele na Idaho umefanyika ambapo Jumla ya miche 58,800 imezalishwa na walengwa wa kaya maskini na kupandwa na kaya hizo zinazonufaika na TASAF awamu ya III kwa kila mlengwa kupanda ekari 2 za mikorosho	-Baadhi ya wakulima kutofuata kanuni bora za zao la Korosho